## EPISODE 1: "MUST HAVE AN INTERNET CAFÉ!"

| | |
|---|---|
| **SCRIPT WRITER** | **Njoki Muhoho** |
| **EDITOR** | **Jan-Philipp Scholz** |
| **KISUAHELI:** | **Eric Ponda** |

**CHARACTERS**

| | |
|---|---|
| **ANNOUNCER** | Male Adult |
| **ZAPCOM** | A 23 year old computer geek, by village standards. |
| **GEORGE** | 20 years old. Waits tables at his Uncle Kilu's restaurant. |
| **MUMBI** | 22 years old, Zapcom's cousin and social worker. Female. |
| **OMWA** | 19 years old. Secondary school leaver. Female. |
| **UNCLE KILU** | 55 years old. George's uncle, owner of KULA TU FOODS. |
| **MANAGER** | 45 years old, the local government Telecommunications company manager. Everyone calls him The Manager. |

**<u>INTRO</u>**

1. **<u>MUSIC: THEME MUSIC</u>**

***2.*** **ANNOUNCER** HUJAMBO MPENZI MSIKILIZAJI NA KARIBU KATIKA MFULULIZO WA MAKALA NYINGINE YA MCHEZO WA REDIO 'LEARNING BY EAR' NOA BONGO JENGA MAISHA YAKO, TUKIANGAZIA

ENZI YA TEKNOLOJIA MPYA YA HABARI NA MAWASILIANO. KATIKA MCHEZO HUU WA LEO KWA JINA ***"MKAHAWA WA INTANETI'.***

**3. ANNOUNCER** KUTUNA NA ZAPCOM, MTAALAM WA MASUALA YA KOMPUTA NA RAFIKI MKUBWA WA GEORGE TANGU UTOTONI. USWAHIBA WAO WA JADI SASA NI KAMA CHANDA NA PETE. ZAPCOM ANAMTEMBELEA SHANGAZIYE , AFISA MENEJA WA MASUALA YA TEKNOLOJIA YA MAWASILIANO YAANI ICT JIJINI. NA AMEPENDA SANA MASUALA YA TEKNOLOJIA MPYA YA HABARI NA MAWASILIANO. KWA UPANDE WAKE GEORGE, ANAENDELEA NA KAZI YAKE KIJIJINI KATIKA MKAHAWA WA CHAULA WA KULA TU FOODS UNAOMILIKIWA NA BABAKE MDOGO. NI KIJANA MCHESHI MWENYE BIDII NA ANAYEPENDA KAZI YAKE LAKINI HANA HABARI KUHUSU YALE YANAYOENDELEA NJE YA KIJIJI CHAO. JE ZAPCOM KIJANA MWENYE MAJIVUNO NA KUJIGAMBA ATAWEZA KUTUMIA UJUZI ALIONAO WA TEKNOLOJIA YA KISASA YA MAWASILIANO KUBADILI MAMBO KIJIJINI MWAKE, NA JE ATAWEZA KUBADILI MAISHA YA SWAHIBA YAKE GEORGE?

**SCENE 1: KULA TU FOODS EARLY MORNING.**

**4. A-SFX: <u>DOOR OPENS, SOUNDS OF AN AFRICAN SMALL LOCAL RESTRAURANT FILL THE AIR</u>**

**5. ZAPCOM** Hamjamboni nyote wapenzi…!

**6. GEORGE** (**VERY EXCITED**) Zapcom! Umerudi !

**7. B-SFX: CROCKERY CLATTER, FAST FEET SHUFFLE AS GEORGE AND ZAPCOM RUSH INTO EACH OTHER, HUGGING AND SLAPPING SHOULDERS.**

**8. ZAPCOM** Zaaaaappp – mtaalam wa Komputa amerudi. Ni furaha yangu kurudi tena hapa nyumba Kula Tu Foods!

**9. GEORGE** Hebu kwanza keti uniambie habari za huko, shangazi yako anaendeleaje na masomo yake, habari za jiji na kadhalika…… kabla babako mdogo kurejea.

**10. . ZAPCOM** Swahiba George, shangazi yangu ni mzima hana neno… alinifadhili kozi nzuri sana kuhusu masuala ya kuunganishwa na mtandao wa Intaneti, jinsi ya kuutumia, kusoma kurasa za blogi, kupiga gumzo na marafiki mtandaoni. Si bure wakiniita ZAPCOM!

**11. GEORGE** Unazungumza lugha gani ?

**12. C-SFX: CHAIRS PULLING IN AND OUT AS THEY SIT DOWN.**

**13. UNCLE KILU** (**SHOUTING FROM A DISTANCE**).
George, hebu toka haraka, sikukuajiri ukae tu ukipiga gumzo na marafiki zako mchana kutwa… Hebu nenda jikoni haraka uoshe vyombo…..

**14. GEORGE** Uncle, mtazame anayekuja?

**15. UNCLE KILU** Sidhani ataweza kukulipa mshahara bila kufanya kazi iliyokuleta hapa ya kuwahudumia wateja. Wewe, Zapu,,…au wanakuitaje siku hizi.……

**16. ZAPCOM** (**INTERRUPTS**) Ni …ZAPP COMMM sio Zapu. (GUSTO) Zapppp yaani kasi na COMM teknolojia mpya ya mawasiliano...

**17. UNCLE KILU** Vyovyote vile, lakini na hakika mamako hakukupa jina hilo….lakini ni sawa …. Kila mara unaporudi kutoka kwa shangazi yako jijini huwa na mawazo mapya yanayomkanganya na kuvuruga akili ya mwanangu ….(**TO GEORGE**). George, kwani mimi sijakufunza heshima na tabia njema? (**EMPHASIS**) Huwezi kupata habari kutoka kwa mtu mwenye njaa, hebu nenda jikoni umwekee rafiki yako angalau kikombe cha chai na vitafunio,sambusa za moto pia. Yaonekana maisha ya jiji hayakufai..umepoteza uzani fulani!

18. GEORGE Ndio mjomba nitarudi baada ya muda mfupi tu

**18. UNCLE KILU** (**CONSPIRATORY WHISPER**). Mwanangu, yote haya unayojifunza hakikisha pia unamfunza rafiki yako. Sina fedha za kutosha kumpeleka shuleni huko jijini. Hivyo wakati unapokuwa hapa jaribu kumfunza mawili matatu, ili naye ajifunze kutoka kwako!

**19. D-SFX: CLATTER OF CUPS AND PLATES ON TABLE.**

**20. UNCLE KILU** Vyema kabisa … umefanya vizuri sana George. Sasa mimi nitawaacha mwendelee na mazungumzo yenu kuhusu maisha ya jiji.

**21. UNCLE KILU** Ehhe George…

**22. GEORGE** Ndio Ba-Mdogo?

**23. UNCLE KILU** Usikawie, kwani wateja bado wanaendelea kuingia hapa.

**24. GEORGE** Ndio Ba-mdogo. (**TO ZAPCOM**). Sasa niambie habari za jiji. Na hamu sana kusikia yote.

**25. UNCLE KILU** Jambo jingine George…!

**26. GEORGE** (**IMPATIENT**) Ndiooooo Ba Mdogo?

**27.** **UNCLE KILU** Hata werevu pia husikiliza…. Kumbuka una masikio mawili.

**28.** **ZAPCOM** Sawa, Mzee, tutajiribu kufunzana. Hata wewe unapasa kujifunza mambo haya ya teknolojia mpya ya habari na mawasiliano, yaani intaneti.. hebu keti hapa na sisi…

**29.** **UNCLE KILU** (**MUMBLING AS HE WALKS AWAY**)….. Tangu lini ukaona mbwa wazee kujifunza mbinu mpya?

**30.** **ANNOUNCER** Kama ilivyo desturi yake ya majivuno na majigambo, na kwa wepesi Zapcom anamgeukia George na kumueleza kuhusu ujuzi wake. George anachanganyikiwa kama kondoo aliyenyeshewa. Mwalimu huyu na mwanafunzi wake wanapata mgeni wa ghafla, pia rafiki wao wa muda mrefu.

**(MUSIC BRIDGE)**

**SCENE 2: KULA TU FOODS LATER IN THE MORNING**

**31.** **E-SFX: SNIFFING, SHUFFLING**

**32.** **ZAPCOM** OMWA!? Mbona waonekana umedhoofika sana na mwenye kukata tamaa... kuna shida gani? Nini kinachokukasirisha asubuhi hivi na mapema?…Na nini kinachokuleta hapa mkawaha wa Kula Tu Foods wakati kama huu?

**33.** **OMWA** Nimepoteza kazi yangu!

**34. ANNOUNCER** INAVYOONEKANA NI KWAMBA MKAHAWA HUU WA MZEE KILU NDIPO MAKUTANONI KWA WATU MASKINI, WALIOKATA TAMAA,NA WENYE FURAHA PIA KUJA KUVINJARI. OMWA MKAAZI WA KIJIJI HICHO AMBAYE AMEHESHIMIKA NA PIA WENGINE KUMUONEA KIJICHO KUTOKANA NA KAZI YAKE KAMA AFISA MSIMAMIZI KATIKA BARAZA LA MJI, SASA BILA SHAKA MAISHA YAMEMBADILIKIA BAADA YA KUACHISHWA KAZI. LAKINI NI KWA NINI?

**35. ZAPCOM** Hebu ngoja kidogo .. umefutwa kazi baada ya kuanzishwa huduma za Komputa.

**36. OMWA** Umejuaje?

**37. ZAPCOM** Kwa wewe umepitwa na wakati hujishughulishi kabisa na masuala ya teknolojia mpya au kujifunza mambo ya Komputa. Unahitaji kwenda na wakati Omwa!

**38. GEORGE** Zap! Usiwe bahili.

**39. ZAPCOM** Sio kuwa bahili, ni ukweli. Mambo yamebadilika siku hizi, Ulimwengu umekuwa kama kijiji, enzi ya kuishi kama kijiji barani Afrika imekwisha, sasa lazima tendwe na wakati, ambapo sekta ya mawasiliano imeboreshwa na watu wanabadilishana habari kwa kasi sana. Omwa siku hizi si lazima ukalie mashini ya kupiga chapa kuandika ripoti yako, kisha uende hadi posta kutuma ripoti hiyo…..hapana! amkeni, amkeni ……tubadilke na wakati.!

**40. OMWA** Sasa unataka nifanye nini? Sina pesa za kugharamia mafunzo ya komputa.

**41. ZAPCOM** Unachohitajika kwanza ni kuonyesha ari ya kujua kinachoendelea ulimwenguni. Bila kufanya hivyo utajikuta kama sanamu katika makavazi ilhali wewe bado kijana mdogo chini ya umri wa miaka 25 !

**42. F-SFX: SOUND OF CHAIR BEING PULLED OUT.**

**43. MUMBI** Tangu lini wewe umekuwa na busara hizi, Zapcom?

**44. ZAPCOM** Ah…Kaka Mumbi! hata huna haya kutunyemelea hivyo?.

**45. ANNOUNCER** KWA KWELI MKAHAWA HUU UMEKUWA MASKANI YA VIJANA KUKUTANA. MUMBI, BINAMUYE ZAPCOM PIA AMEPITIA KUPATA ANGALAU KIKOMBE CHA CHAI NA KUBARIZI BAADA YA KAZI NA KUPIGA GUMZO NA ZAPCOM.

**(MUSIC BRIDGE)**

**SCENE 3: KULA TU FOODS. LATE MORNING**

**46. G-SFX: FOOTSTEPS TOWARDS THEM.**

**47. UNCLE KILU** Natumai mazungumzo yenu yatatuletea fedha zaidi katika mkahawa huu wa Kula Tu Foods. Yanonekana hata George amepata amepumzika kidogo kazini.

**48. GEORGE** Ohh, pole sana Ba-mdogo.

**49. MANAGER** (**FROM THE BACK OF THE ROOM**) Tafadhali tunaweza kuhudumiwa hapa?

**50. UNCLE KILU** (**IN PANIC**). Ni meneja wa mawasiliano! George, nenda haraka ukamuhudumie upesi!

**51. MUMBI** (**WHISPERING**) Yuko hapa…? Zapp, hebu tuzungumze naye. Si umepata hizi habari kwamba kijiji chetu kitaunganishwa na mtandao wa Intaneti? Basi kama meneja mwenyewe wa mawasiliano yupo hapa, ni vyema kumuuliza, ama wasemaje? Nahitaji sana huduma hizi za Intaneti kwa kazi zangu.

**52. ZAPCOM** Basi twende tumuulize…

**53. OMWA** Hatuwezi kwenda sasa, bado anakula!

**54. ZAPCOM** (**IGNORING HER**) Tunachohitaji ni komputa na kuunganisha na huduma za intaneti kwa njia ya isiyotumia nyaya*,* na hivyo tunahitaji ushauri wake. (**SHOUTING ACROSS**) Habari za asubuhi Bw meneja! Ni kweli kwamba hivi karibuni kijiji hiki kitaunganishwa na huduma za Intaneti?

**55. MANAGER** (**FROM ACROSS AND MOUTH FULL**) Kwa nini unaniuliza swali hilo kijana?

**56. ZAPCOM** Tunataka kuanzisha mgahawa wa huduma za Intaneti…. Hapa katika mgahawa huu wa Kula Tu Foods.

| | | |
|---|---|---|
| **57.** | **UNCLE KILU** | Zepu, unawazimu wewe? Tayari nina mgahawa wa kuuza chakula hapa, sitaki biashara nyingine hapa? |
| **58.** | GEORGE | (**LAUGHING**). Si mgahawa wa chakula Ba-mdogo… |
| **59.** | **H-SFX: FEET APPROACHING** | |
| **60.** | **MANAGER** | Nafurahi sana kuona vijana kama nyinyi mnafuatilia sana maendeleo ya mawasiliano. Nimefurahi sana tena saana! |
| **61.** | **UNCLE KILU** | Bw usimjali yule … wale …. Wanaa…. |
| **62.** | **MANAGER** | La hasha ni vijana wa kizazi cha sasa wanaotilia maanani na kufuatilia sana masuala ya habari na mawasiliano. Tunapasa kuwasikiza. Kuna mambo mengi tu ya kujifunza. |
| ***63.*** | **OMWA** | (**WHISPERING**) Nini maana ya ***wireless?*** |
| **64.** | **MANAGER** | Msichana, ***wireless*** ni huduma za mawasiliano au kubadilishana habari kwa njia ya intaneti au kuunganishwa bila ya kutumia nyaya. Huduma hii inaweza kutumiwa na wenye komputa na pia simu za rununu kuwasiliana. |

.

| | | |
|---|---|---|
| **65.** | **GEORGE** | Lakini … Zapcom, si hiyo uliniambia ni Intaneti? |

**66. MUMBI** Kwa kujibu swali lako. Huduma za Intaneti zinapatikana kote ulimwengunu. Ni mtandao wa ulimwengu mzima unaounganisha komputa, na kuwawezesha wenye kutumia mitambo hii kuunganishwa na kutuma na kupokea habari. Pia unaweza kutumia huduma hizi kupitia simu yako ya mkononi.

**67. GEORGE** Oooh,kumbe!. Kwa hiyo kwanza nahitaji kuwa na Komputa, kisha huduma hizi za Wireless, ili niweze kuunganishwa na intaneti?

**68. J-SFX: CLAPPING AND CHEERING BY ALL.**

**69. MANAGER** Mmm, nimefurahi sana. Kwamba wewe ni kijana mwerevu anayeshika mambo haraka George. Na kuhusu simu za mkononi,…. nilisikia ukitaja.

**70. GEORGE** Hapo kidogo nimechanganyikiwa.

**71. OMWA** (**SOUNDING BORED**). Kwa vile mimi na Komputa ni kama pamba na moto, labda naweza kuelewa haraka mambo ya simu za mkononi.

**72. K-SFX: SHUFFLE OF CLOTHES AND CHAIRS .**

**73. MANAGER** Sikiza hapa, si lazima utumie Komputa kuunganishwa na huduma hizi. Pia unaweza kutumia simu yako ya mkononi. Hebu tazama hapa…. unaona ….

**74. L-SFX: CHAIRS CREEK AS THEY MOVE CLOSER.**

**75. OMWA** (**FOR ONCE JOYOUS**). Simu ya mkononi?...naweza kutumia hiyo pia !

**76. ZAPCOM** Lakini unahitaji simu ambayo inaweza kuunganishwa na huduma hizi za Intaneti kwa urahisi! Hata hivyo (**DREAMILY**) mbona sioni sahani ya George hapa Ba-Mdogo Kilu. Naona tu komputa, na mngurumo wa vifaa vya komputa yaani ***hard-drives*** ,na nyinyi mkiendelea kubonyeza herufi kwenye kibao cha komputa yaani, ***keyboards*** mnapobadilishana habari na ulimwengu mzima. … (**MORE EXCITED**) Kumbe……!

**77. I-SFX: CHAIR BEING PULLED BACK. SHUFFLE OF FEET**

**78. MANAGER** (RUSHED). Oh, hebu tazama ni saa ngapi! Napasa kurudi ofisini.

**79. MUMBI** (**REPREMANDING**). Zap, unaona ndoto yako ilipotufikisha? Bw Meneja anataka kuondoka sasa!

**80. MANAGER** (**DISMISSIVE**) Hapana, hapana, endeleeni na ari hiyo vijana. Wale wote wasio na matarajio au ndoto hukosa muelekeo maishani……

**81. ZAPCOM** (**STILL IN DREAMLAND**)...Sasa macho yote yako kwa komputa, mnapoendelea kubadilishana habari. …

**82. MANAGER** (**CONTINUES**)……Kwa nini usizungumze na sekretari wangu, ili tunaweza kupanga wakati mzuri wa kujadilia suala hili kwa kina.

**83. MUMBI/GEORGE/OMWA** Asante sana, asante sana Bw Meneja.

**84. ZAPCOM** … (**CONTINUES DREAMING**)…Akifungua komputa yake na kuanza kusikiliza muziki, na kutazama picha. ……….

**85. MUMBI** (**INTERRUPTING**) Tosha, tosha Zapcom!!!

**86. ZAPCOM** (**ABRUPTLY**). Nini , eti nifunge komputa? Lakini ni ***LAZIMA*** tufungue mgahawa hapa!

**MUSIC: THEME MUSIC**

**OUTRO**

**87. ANNOUNCER** Sasa kijiji hicho cha mashambani kitaweza kuunganishwa na ulimwengu wa mawasiliano. Hii ni iwapo tu fikra na mawazo ya ZAPCOM na rafiki zake yatafaulu na kuweza kufungua mkahawa wa kutoa huduma za Intaneti kijijini . Lakini kwa kuzingatia changamoto ya ukosefu wa elimu na rasilimali za kutosha , je watafaulu.?Na je Ba-Mdogo Kilu atawakubalia kufungua mkahawa wao mahali hapo? Ungana nasi tena kwa makala yajayo ufahamu kitakachoendelea. Pia unaweza kutembelea mtandao wetu wa www.dw-world.de/lbe kwa maelezo zaidi kuhusu vipindi vyetu vya LEARNING BY EAR NOA BONGO JENGA MAISHA YAKO.

Pia ukiwa na maoni usisite. Hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa.